MKAKATI WA UWAZI WA TASNIA YA UZIDUAJI

Muongozo thibitisho

Yaliyomo

1. Utangulizi 3
Dhumuni la uthibitisho 3
Mtazamo wa udhibitishwaji 4
2. NYARAKA MUHIMU KATIKA MCHAKATO WA UTHIBITISHO 7
3. Taarifa ya Uthibitishwaji 11
4. Baada ya Uthibitishwaji 12
5. Mfumo wa Uthibitishwaji 14
6. Vyombo Viashirio vya Tathmini 16
7. Fomu za Kampuni 31
8. Kiashirio cha Mapitio 36

1. Utangulizi

Dhumuni la uthibitisho

Kuna madhumuni mawili ya uthibitisho:

- Nchi ambazo zinatekeleza EITI, lakini hazijakamilisha utekelezaji wa EITI (Nchi wanachama- angalia jedwali Na., hapa chini) uthibitisho unapashwa kupima maendeleo ya utekelezaji.
- Nchi ambazo zimekamilisha utekelezaji wa EITI (Nchi zilizotimiza masharti- angalia jedwali Na….. hapa chini), Uthibitisho unapaswa kutoa tathmini kamili ya kanuni na vigezo vya EITI kwa nchi zote zilizotimiza masharti.

Kama ilivyoonyeshwa hapo juu makundi mawili ya nchi tofauti yalikubaliwa:

Nchi tahiniwa ni zile nchi ambazo zimekubali kutekeleza matakwa ya EITI na kutimiza masharti ya viashirio vinne katika hatua ya kujiandikishakwenye mfumo wa uthibitishaji. (Angalia jedwali Na.… hapo chini)). Hii ina maana ya kukubali kutekeleza matakwa yote ya EITI; vile vile kukubali kufanya kazi na vyama vya ushirika na sekta binafsi, kuteua mtu kuongoza utekelezaji wa EITI; na Kuandaa mpango wa kazi unakubaliwa na wadau wote kazi uliokubalika na wadau.

Nchi zinazotekeleleza matakwa ya EITI ni zile nchi ambazo zinatekeleza matakwa ya EITI. Nchi ambazo zimetimiza viashirio vyote katika mfumo wa uthibitishwaji, inabidi zichapishe na kusambaza taarifa zake kwa EITI.

Mtazamo wa udhibitishwaji

Mchakato mzima wa udhibitishwaji, umefafanunuliwa zaidi pamoja na hatua zilizokubaliwana kuwekwa kwenye muongozo huu.

Hatua ya kwanza ni kundi la washikadau kumteua Mdhibiti, Mthibiti anayechaguliwa atatakiwa kutumia nyaraka tatu katika kutekeleza kazi zake ambazo ni:-

- Mpango kazi wa nchi husika
- Vyombo vya uthibitisho vya mfumo wa uthibitishaji viashirio tathmini, na
- Fomu za kampuni

Kwa kutumia nyaraka hizi mthibiti hukutana na kundi la wadau na shirika lililochaguliwa kupitia mahesbau ya makampuni yaliyowasilisha mahesabu, pamoja na mahesabu yaliyowasilishwa na serikali na mashirika yasiyokiuwa ya kiserikali.

Kwa kutumia maelezo haya, Mthibiti ukamilisha taarifa, yenye kujumuisha:-

- Taarifa fupi ya maendeleo dhidi ya Mpango Kazi wa Nchi

- Taarifa fupi ya maendeleo dhidi ya viashirio katika mfumo wa uthibitishwaji
- Mfumo wa uthibitishwaji uliokamilika
- Taarifa ya utekelezaji ya kampuni
- Fomu za kampuni zilizounganishwa
- Tathimini ya jumla ya utekelezaji wa EITI: Je nchi tahiniwa , na inafuata masharti au haina maendeleo yenye manufaa

Taarifa hii uwasilishwa kwa kundi la washikadau, serikali na Bodi ya EITI. Kama haya makundi yameridhika na taarifa ya uthibitisho inachapishwa, hitimisho na mapendekezo hufanyiwa kazi

Kama kuna kutokukubaliana kuhusiana na mchakato wa uthibitisho, kazi hii kwanza hushughulikiwa na watu wa ndani na Bodi ya EITI uhusishwa kama panaibuka migogoro yenye utata zaidi..

Uthibitisho si ukaguzi wa hesabu za fedha.Ila kazi ya Mthibiti ni kuangalia nchi na kampuni kama zinafanaya kazi kama inavyotakiwa na siyo kufanya ukaguzi wa fedha.

Umbo 1: Jedwali la mtiririko wa uthibitisho


Mthibiti anateuliwa na kundi la wadau mbalimbali
Uthibitisho kuanza
Mpango kazi wa nchi
Mfumo wa Uthibitishaji
Fomu za kampuni
MSG
Mashirika yanayofanya usuluhisho wa EITI
Wawakilishi wengine wa serikali
Vyama vingine vya jamii
Makampuni Mengine
Ripoti
Bodi ya EITI
serikali
MSG
Imekubalika ?
Iliyochapishwa
Serikali / MSG zikifanyia kazi mahitimisho

2. NYARAKA MUHIMU KATIKA MCHAKATO WA UTHIBITISHO

Mpango Kazi wa Nchi

Nchi inayotekeleza mpango kazi wake ina umuhimu wa pekee katika mchakato mzima wa uthibitishwaji .Mpango kazi lazima utimizwe na kuchapishwa kabla ya nchi husika hazijasaini mikataba ya maadalizi. Vigezo vya EITI vinahitaji kuwa na mpango kazi endelevu kifedha na hivyo ujumuishe yafuatavyo:-

- Malengo yanayopimika
- Ratiba ya utekelezaji
- Na tathmini ya matatizo yanayoweza kujitokeza

Mpango wa kazi hauna budi kuonyesha pia jinsi serikali itakavyohakikisha ushirikishwaji wa wadau wa aina mbalimbali wa EITI, hususani ushirikishaji wa vyama vya Ushirika.

Mpango wa kazi utaonyesha raatiba za uthibitisho wakati nchi ikiwa bado ni tahiniwa. Hii itasaidia kuonyesha mahitaji halisi ya nchi na mpango kazi utatakiwa kufanyika mara moja kila baada ya miaka miwili., Bodi ya EITI yaweza kuweka utaratibu wa uthibitishwaji wa mara kwa mara unaoweza kusaidia nchi tahiniwa kutekeleza EITI bila ya usumbufu. Mpango wa kazi unapaswa kufafanua, jinsi serikali itakavyolipia uthibitishwaji.

Mthibiti atahitaji kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa EITI dhidi ya malengo na ratiba na kutathmini kama nchi imechambua na kuyafanyia kazi matatizo yaliyokuwa yameanishwa kabla.

Jambo la la msingi katika kuhakikisha uthibitishwaji wa nchi unafanyika itakuwa ni kama nchi husika inafuata ratiba ya utekelezaji kama ilivyopangwa. Kama ratiba haifuatwi, Mthibiti kwa kuwasiliana na wadau wengine ndio utakuwa ushaidi tosha wa kuamua kama ucheleweshaji wa kutofuata raiba ya utelezaji una maana.

Maendeleo ya utekelezaji wa EITI lazima yaonyeshwe kwenye ripoti.

Mfumo wa Uthibitishwaji wa EITI na vigezo vya kutathmini Viashirio

Kimsingi mchakato wa uthibitisho ni mfumo wa uthibitishwaji. Hii inahusisha viashirio 20 ambavyo hutumiwa na mthibiti kutathimini maendeleo. 18 kati ya hivyo vitapaswa kutathminiwa kama ilivyopangwa au isivyopangwa kwenye boksi la vema. Viashirio viwili (Uthibitisho wa kampuni na Mapitio) vitatathminiwa katika taarifa ya mthibiti. Taarifa ya mthibiti inapaswa kujumuisha mfumo wa uthibitishwaji na vigezo vya Viashirio vya Tathmini (angalia kiambatisho Na….) na vilevile taarifa ya maendeleo dhidi ya viashirio.

Takribani nusu ya viashirio katika mfumo wa uthibitishwaji ni muhimu na huitaji mthibiti kuona kama Vimefuatwa au la.

Nusu ya viashiria iliyobaki ni muhimu kidogo, na inahusisha mambo yafuatayo:-

a. **Kiashirio Na.4 Mpango Kazi wa Nchi**. Kama ilivyoelezwa hapo juu, Mpango Kazi wa Nchi ni sehemu muhimu ya mchakato wa uthibitishwaji. Kwa sababu ya hiyo kiashirio cha Na. 4 katika Mfumo huu unahusisha vigezo vya viashrio vinavyotumika kutathimini sehemu ya mpango kazi wa nchi.

b. **Hatua ya utayarishaji**. Tathmini ya maendeleo inayofanywa na mthibiti katika maandalizi ya awali itahusisha hatua mbali mbali za utekelezaji katika nchi tofauti. Mpaka sasa kila kiashirio kinajumuisha vigezo vya viashirio namna ya kutathimini viashirio ambavyo vinatoa muongozo kwa mthibiti jinsi ya kutathmini kiashirio.

c. **Uthibitishwaji wa Kampuni**. Hii ni sehemu ya mchakato wa uthibitishwaji wa nchi, lakini huitaji majibu kwa maswali ambayo yanalenga shughuli za kampuni katika nchi husika. Kampuni inatakiwa kujaza fomu za kujitathimini yenyewe. Hamna boksi la vema kwenye mfumo katika uthibitisho wa kampuni hivyo innakuwa vigumu kuwa na muhtasari wa taarifa za kampuni nyingi kwa kampuni inayotimiza masharti au la. Aidha, Mthibiti inampasa ajumuishe mapitio ya makubaliano ya kampuni katika taarifa zake, na vilevile kuambatanisha jedwali la makubaliano kwenye ripoti ya uthibitishwaji.

d. **Utoaji**, Tathmini ya taarifa ya uthibitishwaji ni lazima iwekwe wazi kwa uma

e. **Mapitio**, yanayopelekea malengo bora kwa ajiri ya mapitio.

Kama ilivyoelezwa hapo juu **vifaa vya viashirio vya tathmini** vimendelezwa kama viashirio maalum. Madhumuni ya **viashirio vya tathmini ni kwa ajili ya kutoa** muongozo wa ziada kwa Mtathmini katika hali ambayo viashirio vimehusishwa au kudhaniwa.. Kwenye baadhi ya IATs Mthibiti anapaswa kuhakikisha kila sehemu ya ushahidi iliyoandikwa inaonekana. Kwa IATs nyinginezo chombo uonyesha kuwa kuna njia tofauti ambazo nchi yapaswa kuchukua na ushahidi ulioandikwa uwe umechanganuliwa. Kwa hizo IATs , sio muhimu kuona kila sehemu ya ushahidi iliyoandikwa kutathmini kiashirio inakubalika.

Fomu za Kampuni

Utekelezaji wa kampuni EITI hauna budi kuthibitishwa. Hii inatokea hasa kama sehemu za uthibitisho wa nchi. Kwa hiyo mchakato wa uthibitisho wa nchi una fomu za tathmini binafsi kwa ajili ya kampuni kujaza na kurudisha kwa Mthibiti. Mthibiti ana mamlaka ya kuuliza maswali kampuni kwa maelezo ya kusaidia zaidi kama ni muhimu.

Fomu zilizokamilika zitatumwa kwa njia ya tovuti ya kampuni na taarifa ya uthibitisho itakuwa na jedwali lililounganisha fomu za tathmini binafsi za kampuni.

Endapo kampuni itashindwa kukamilisha kujaza fomu za tathmini binafsi, Mthibiti ataonyesha hili katika taarifa ya tathmini, na kujumuisha katika taarifa maelezo yote yanayohusu kampuni husika kwa uma Kampuni itaruhusiwa kupitia taarifa zilizoandikwa.

Kampuni zinazoshiriki katika EITI zitatakiwa kuwa zimeidhinishwa katika tovuti za mtandao wao.

Kampuni ambazo zimefanya makubaliano ya kimataifa kusaidia EITI zitajaza fomu za kampuni za ngazi ya kimataifa za tathmini binafsi, ambazo zitatumwa moja kwa moja kwa EITI sekretarieti. Hizi zitatumwa kwa njia ya mtandao wa EITI.

3. Taarifa ya Uthibitishwaji

Kama ilivyoelezwa hapo juu, taarifa ya uthibitishwaji ina mambo yafuatayo:-

- Taarifa fupi za maendeleo dhidi ya Mpango Kazi wa Nchi
- Taarifa fupi za maendeleo dhidi ya viashirio vya mfumo wa udhibitishwaji
- Mfumo wa udhibitishwaji uliokamilika
- Taarifa ya utekelezaji wa kampuni
- Fomu za kampuni zilizounganishwa

- **Tathmini ya jumla ya utekelezaji wa EITI: Ni nchi tahiniwa, nchi inayotekeleza mashartii au hakuna maendeleo ya maana ?**

Aidha ni muhimu kuwa, uthibitishwaji unaonyesha kwamba hamna maendeleo muhimu yamefanyika, na kuna nia ndogo ya utekelezaji EITI pamoja na kanuni na vigezo, Mthibiti atatoa tathmini iliyo wazi na itakayoiwezesha bodi kutoa maamuzi ya kuzitoa nchi kutoka kwenye orodha ya nchi wanachama. Kabla ya kufanya mapendekezo kama haya Mthibiti uhakikisha kwamba nchi imepata muda wa kufuatilia utafiti kama huu. Hii yaweza kumaanisha, kwa mfano, mapendekezo kama hayo yangethibitishwa kwa kufuatilia tu mazoezi mawili ya uthibitishaji ambapo kila moja limefikia hitimisho linalofanana. Hata hivyo katika hali nyingine yaweza kuwa sawa kuwa na hitimisho kama hilo baada ya kuwa na uthibitisho mmoja tu.

Taarifa pia itakuwa na somo lililofundishwa, vilevile na ushauri uliotolewa na watu, na mapendekezo kwa utekelezaji wa baadaye wa EITI.

Endapo taarifa imekubaliwa na kundi la wadau mbalimbali, serikali na bodi ya EITI, itachapisha kwa lugha ya Kiingereza na kiswahili.

4. **Baada ya Uthibitishwaji**

Endapo kutakuwa na kutokubaliana kati ya EITI, serikali, na wadau wengine au Bodi ya EITI juu ya Taarifa ya Mthibiti itashughulikiwa kwanza na Mthibiti anayefanya kazi na kundi hili.

Kama kutokubaliana kunawezekana kutatatuliwa. Mthibiti hana budi kufanya marekebisho kamili katika Taarifa. Kama kutokubaliana hakuwezi kutatatuliwa, itaonyeshwa katika taarifa ya Mthibiti.

Kutokubaliana kabisa kuhusu mchakato wa uthibitisho itabidi kuwasilishwa kwenye ya Bodi ya EITI na Mwenyekiti atahusika kusuluhisha mgogoro huo. Bodi na Mwenyekiti wana mamlaka ya kukataa malalamiko ambayo wanafikiri ni ya kipuuzi, uchokozi au yasiyothibitishwa.

5. Mfumo wa Uthibitishwaji

Vigezo vya EITI-

Utekelezaji wa EITI lazima ukubaliane na vigezo vifuatavyo

1. UCHAPISHAJI: Malipo yote ya uchapishaji wa mara kwa mara wa nyaraka za mafuta, gesi na madini yanalipwa serikalini (Malipo) na mapato yote ya bidhaa (Nyaraka) za kampuni za mafuta, gesi na madini (Mapato) to wide audience in a publicly accessible, comprehensive and comprehensible manner

2. UKAGUZI:Ambapo wakaguzi hawajawahi kuwepo, malipo na mapato yanategemea uaminifu wa ukaguzi wa hesabu unaojitegemea, unaotumia viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa hesabu.

3.USULUHISHAJI/ULINGANISHAJI: Malipo na mapato yanasuluhishwa na mtawala mwaminifu na asiye tegemezi, anayetumia viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa hesabu, na uchapishaji wa maoni ya mtawala yanayozingatia kuwa usuluhisho unajumuisha hitilafu zozote, hazina budi zote kutambuliwa.

4. UPEO: Njia hii inahusisha kampuni zote zikiwemo kampuni zinazomilikiwa na serikali.

5. VYAMA VYA USHIRIKA: Vyama vya ushirika kwa kweli vinashirikishwa kihai katika kubuni, kusimamia na tathimini ya mchakato huu, na kuchangia kwenye

Utekelezwaji wa EITI

Uandikishaji

1. Serikali imetoa maelezo (kamilifu) kwa nia yake ya utekelezaji wa EITI? ☐

2. Serikali imekubali kufanya kazi na vyama vya Ushirika na makampuni katika utekelezaji wa EITI? ☐

3. Serikali imeteua kiongozi wa juu wa utekelezaji wa EITI? ☐

4. Ina mpango wa kazi unaoonyeshagharama uliochapishwa na unapatikana kwa uma, unaojumuisha malengo yanayopimika, ratiba ya utekelezaji, tathmini ya vikwazo vya uwezo. (Serikali, sekta binafsi na vyama vya kijamii)? Angalia kiashiria ukaguzi (IAT) ☐

Utayarishaji

5. Serikali imeanzisha kundi la wadau mbalimbali kusimamia utekelezaji wa EITI? Ona IAT ☐

6.Vyama vya ushirika vimeusishwakatika mchakato? Ona IAT ☐

7.Kampuni zimeusishwa katika mchakato? Ona IAT ☐

8. Serikali imeondoa vikwazo vyovyote katika utekelezaji wa EITI? Ona IAT ☐

9. Imekuwa ikitaarifu violezo vilivyokubaliwa? (Ona IAT ☐

	Ufichuaji	Usambazaji
10. Yaliyomo katika kamati ya wadau yameteuliwa na ushirika kulinganisha mahesabu? Ona IAT ☐	14. Malipo ya bidhaa zote za mafuta, gesi na madini yaliyofanywa na makumpuni kwa serikali yaliarifiwa kwenye shirika yalipoafikiwa kusuruhisha/ kulinganisha mahesabu na kutoa ripoti ya EITI? ☐	18. Taarifa ya EITI iliwekwa bayana kwa uma kwa namna iliyokuwa: -Inafikiwa na uma -Pana na -Yakueleweka? Ona IAT ☐
11.Serikali imehakikisha kampuni zote zitatoa taarifa? Ona IAT ☐	15. Mapato ya bidhaa zote za mafuta, gesi na madini iliyopata serikali yaliarifiwa kwenye shirika yalipoafikiwa kusuruhisha/ kulinganisha mahesabu na kutoa ripoti ya EITI? ☐	
12. Serikali imehakikisha kuwa ripoti za makampuni zinatokana na hesabu zilizokaguliwa kwa viwango vya kimataifa? Ona IAT ☐	16. Kundi la wadau mbalimbali limehusisha kuwa Shirika lililoafikiwa kusuluhisha/ kulinganisha hesabu za kampuni na serikali zimefanywa inavyotakiwa? ☐	
13. Bidhaa zote za mafuta, gesi na madini zinalipwa na kampuni serikalini kwa kuarifiwa kwenye shirika yalipoafikiwa kusuruhisha/kulinganisha mahesabu na kutoa taarifa ya EITI? ☐	17. Taarifa ya EITI ilitambua itilafu na kutoa mapendekezo kwa hatua zinazotakiwa kuchukuliwa? Ni jinsi gani makampuni ya mafuta, gesi na madini yameunga mkono utekelezaji wa EITI Angalia IAT	Hatua zipi zimechukuliwa kufuatilia somo lililofundishwa, kushughulikia hitirafu na kuhakikisha EITI ni endelevu? Angalia IAT

6. Vyombo Viashirio vya Tathmini

Mfumo wa Viashiria 4: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Je mpango wa kazi wa nchi unaoonyesha ghalama, wenye malengo yanayopimika, ratiba ya utekelezaji na tathmini ya vikwazo vya kiuwezo (serikali, sekta binafsi na vyama vya ushirika) umechapishwa na kuwezeshwa kupatikana kwa mapana?

Dhumuni: Mpango wa kazi wa nchi ni msingi wa mchakato wa uthibitishaji wa nchi. Kigezo cha sita cha EITI kinahitaji kuwa mpango wa kazi unaotolewa ambao umekubalika na washikadau muhimu wa EITI na unapatikana kwa uma.

Ushahidi: Ili kukipa kiashiri hiki vema, Mthibiti anategemewa kuona ushahidi kuwa mpango wa kazi umekubaliwa na washikadau muhimu na ambao unajumuisha:

- Malengo yanayopimika
- Ratiba ya utekelezaji
- Tathmini ya vikwazo vya uwezo tegemewa
- Jinsi gani serikali itahakikisha asili ya washikadaudau mbalimbali wa EITI, hususani katika uhusishaji wa vyama vya ushirika.
- Ratiba ya uthibitishaji wakati wa hatua ambapo nchi ni mwanachama. Hii itatoa mahitaji ya nchi , lakini itatakiwa kufanyika angalau mara moja kwa miaka miwili.

- Mpango kazi huna budi pia kuchanganua jinsi serikali itakavyolipia uthibitishaji.

Mthibiti atahitaji kutathmini maendeleo juu ya utekelezaji wa EITI unaopingana na haya malengo na ratiba na kutathmini kama nchi imefuatilia vikwazo vya uwezo.

Sehemu muhimu katika mchakato wa uthibitishaji wa EITI ya nchi utakuwa kama ratiba ya utekelezaji inafuatwa. Kama ratiba haifuatwi, Mthibiti- kutokana na ushahidi kutoka kwa wadau na wengineo muhimu - atahitaji kubainisha kama uchelewaji katika kufuata ratiba una mantinki. Kama hauna mantinki Mthibiti atahitaji kuamua kwa kupendekeza kuwa nchi itolewa kwenye orodha ya nchi wanachama.

Mfumo wa Viashiria 5: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Serikali imeshanzisha kundi la wadau mbalimbali kusimamia utekelezaji wa EITI?

Dhumuni: Utekelezaji wa EITI huna budi kusimamiwa na wadau wote wahusika, wakijumuisha sekta binafsi, vyama vya ushirika (Inajumuisha vikundi vinavyojitegemea vya vyama vya ushirika na vinginevyo kama vyombo vya habari na wabunge) na wizara za serikali husika (zinajumuisha serikali iliyoko madarakani). Kundi litakubaliana na hadidu za rejea za uma zilizowazi. Hizi hadidu za rejea zinajumuisha: Uidhinishaji wa Mpango wa kazi wa Nchi kwa kufuatilia masahihisho endapo ni muhimu; kuchagua mkaguzi wa kufanya shughuli za ukaguzi

wa hesabu endapo data zilizotolewa kwa malinganisho na kampuni au serikali hazijawahi kuhusishwa na ukaguzi wa hesabu kwa kiwango cha kimataifa; kuchagua shirika kufanya tena malinganisho; na maeneo mengine kama yalivyoonyeshwa katika Validation Grid.

Ushahidi: Ili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti anatarajiwa kuona ushahidi kuwa kundi la washikadau mbalimbali limeundwa, ambalo linahusisha washikadau wanaofaa na hadidu zake za rejea zinakubaliana na dhumuni.

Ushahidi unajumuhisha:

- Tathmini ya wadau ambao wametekelezewa hivi.
- Maelezo juu ya ushiriki wa kundi la wadau mbalimbali:
  - Ukaribisho wa kushiriki katika kundi ulikuwa bayana na wazi?
  - Wadau wamewasilisha ipasavyo (hii haimanishi kuwa inabidi wadau Wawasilishwe sawa)?
  - Wadau wamejisikia kuwa wamewasilishwa ipasavyo?
  - Wadau wamejisikia kuwa wanaweza kujiendesha kama sehemu ya kamati- inajumuisha kushirikiana na kundi lao la jimbo na wadau wengineo- kuepukana na uchochezi uliokiuka mipaka au usurutisho?
  - Wahusika wa kundi la vyama vya ushirika wanajiendesha na katika mpangilio wa sera, kwa kutotegemea serikali na/au sekta binafsi?
  - Endapo kundi la wahusika limebadilika, kumekuwa na pendekezo lolote la usurutisho au jaribio la kujumuhisha wahusika ambao hawatapinga hali kama hiyo?

  - Wahusika wa kikundi wana uwezo wa kutosha wa kufanya majukumu?
- Hadidu za rejea zinaipa kamati mamlaka juu ya utekelezaji wa EITI? Hizo hadidu za rejea zinatakiwa angalau zijumuishe: Uidhinishaji wa mpango wa kazi wa nchi-kwa kufuatilia masahihisho endapo ni muhimu; kuchagua mkaguzi wa kufanya shughuli za ukaguzi wa hesabu endapo data zilizotolewa kwa malinganisho na kampuni au serikali hazijawahi kuhusishwa na ukaguzi wa hesabu wa kiwango cha kimataifa; kuchagua shirika kufanya tena malinganisho; na maeneo mengine kama yalivyoonyeshwa katika Validation Grid.
- Je maofisa wa juu wa serikali wamewakilishwa kwenye kamati?

Mfumo wa viashiria 6: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Vyama vya ushirika vimehusishwa katika mchakato?

Dhumuni: Hiki kiashirio kinaimarisha kiashirio cha 5. Vigezo vya EITI vinahitaji vyama vya ushirika vinahusihwa kiuhakika kama washiriki katika kusanifu, kusimamia na kutathmini mchakato, hivyo itachangia katika mdahalo wa uma. Hili kufanikisha, utekelezaji wa EITI utahitaji kuhusisha zaidi vyama vya ushirika. Hii itawezekana kwa kupitia kundi la wadau mbalimbali au zaidi.

Ushahidi: Ili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi kuwa serikali, kundi la wadau mbalimbali wa EITI inapobidi,

wametaka kuhusisha wadau wa vyama vya ushirika katika mchakato wa utekelezaji wa EITI. Hii inajumuhisha ushahidi ufuatao:

- kundi la wadau mbalimbali kutowafikia kundi kubwa la vyama vya ushirika, inajumuhisha mawasiliano (vyombo vya habari, mtandao, barua) na vikundi vya vyama vya ushirika na/au muungano (mfano uchapishaji wa ndani ndiyo tunaita muungano), kuwajulisha ni ahadi ya serikali kutekeleza EITI, jukumu la msingi la kampuni na vyama vya ushirika.
- Hatua za kuchukua kutatua vikwazo vya kiuwezo vinavyodhuru ushiriki wa vyama vya ushirika, hata kama vimeahidiwa na serikali, vyama vya ushirika au kampuni.
- Kundi la vyama vya ushirika waliohusika katika EITI hawana budi kuwa wanajiendesha na kwa kufwata mpangilio wa sera, kwa kutotegemea serikali na/au sekta binafsi.
- Kundi la vyama vya ushirika waliohusika katika EITI wapo wazi kutoa mapendekezo yao juu ya EITI bila kikwazo kisichostahili au ushurutishaji.

Mfumo wa Viashiria 7: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Kampuni zinahusishwa katika mchakato?

Dhumuni: Hiki kiashirio kinaimarisha kiashiria cha 5. Utekelezaji wa EITI unahitaji kampuni zihusishwe katika utekelezaji na hivyo taarifa zote za kampuni ziwe chini ya EITI. Ili kufanikisha adhma hii, utekelezaji wa EITI

utahitaji kujihusisha zaidi na kampuni za mafuta, gesi na madini. Hii itawezekana kwa kupitia kundi la wadau mbalimbali au zaidi.

Ushahidi: Ili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi kuwa serikali, kundi la wadau mbalimbali wa EITI inapobidi, wametaka kuhusisha makampuni ya (mafuta, gesi na madini) katika utekelezaji wa EITI. Hii inajumuhisha ushahidi ufuatao:

- Kundi la wadau mbalimbali Kutoyafikia makampuni za mafuta, gesi na madini na, inajumuhisha mawasiliano (vyombo vya habari, tovuti, barua), kuwajulisha ni ahadi ya serikali kutekeleza EITI, na jukumu la msingi la kampuni.
- Hatua za kuchukua kutatua vikwazo vya uwezo (capacity constraints) vinavyodhuru kampuni, hata kama vimeahidiwa na serikali, vyama vya ushirika au kampuni.

Mfumo wa Viashiria 8: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Serikali iliondoa vikwazo vyovyote katika utekelezaji wa EITI?

Dhumuni: Endapo sheria, kanuni au vikwazo vingine vinatokea juu ya utekelezaji wa EITI, itakuwa muhimu kwa serikali kutoa hivi vikwazo vya kawaida Vikwazo vya kawaida vinahusisha sharti la siri katika mikataba ya serikali na kampuni na kugombanisha idara za serikali za msamaha.

Ushahidi: Hili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi ambao serikali imeondoa vikwazo vyote. Hii yapaswa kufuatuatilia tathmini ya haraka ya vikwazo, au kwa vitendo vya upingaji ili kuepusha vikwazo vitokeapo. Hakuna namna moja ya kushughulikia hili suala- nchi itakuwa na miundo mbalimbali ya kisheria na makubaliano mengine ambayo yaweza kuathiri utekelezaji, na itabidi ishawishike kwa hivi katika namna tofauti.

Aina ya ushahidi Mthibiti atahitaji kujua ungeliweza kujumuhisha:

- Uhakiki wa muundo wa kisheria.
- Uhakiki wa muundo wa uthibiti.
- Vikwazo vya tathmini katika miundo ya kisheria na uthibiti ambayo yaweza kuathiri utekelezaji wa EITI.
- Sheria iliyotungwa au kupendekezwa au mabadiliko ya uthibiti yamebuniwa kuwezesha uwazi.
- Hati ya kusamehe madai ya masharti ya siri yenye mkataba kati ya serikali na kampuni wa kuruhusu ufichuaji wa mapato.
- Mawasiliano ya moja kwa moja kwa mfano Kampuni, zinaruhusu uwazi mkubwa.
- Tamko la maelewano lililenga viwango vya uwazi vilivyokubalika na matarajio kati ya serikali na makampuni.

Mfumo wa Viashiria 9: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Mifumo ya kuripoti imekubalika?

Dhumuni: Mifumo ya kuripoti ni muhimu kwa mchakato wa ufichuaji na ulinganishaji, na utoaji wa taarifa ya mwisho ya EITI. Kiolezo kitafafanua ni aina gani ya mkondo wa mapato imejumuhishwa katika ufichuaji wa kampuni na serikali. Kiolezo kitahitaji kukubaliwa na kundi la wadau mbalimbali.

Vigezo vya EITI vinahitaji kuwa" bidhaa zote za mafuta, gesi na madini zilipiwe serikalini" na mapato yote ya bidhaa za mafuta, gesi na madini ya kampuni yaliyopokelewa na serikali yachapishwe. Kiolezo cha EITI vitahitaji, kwa hiyo, kufafanua kwa makubaliano ya kundi la wadau mbalimbali haya malipo na mapato ya bidhaa yana nini na bidhaa zimeundwa na nini. Itakuwa pia muhimu kwa kundi la wadau mbalimbali kufafanua vipindi vya muda taarifa ipokuwa inatolewa. Mkondo wa mapato ni bidhaa kama ina makosa au haijatoa maelezo yanayotakiwa yaweza kuathiri umuhimu wa ripoti ya mwisho ya EITI.

Kwa kawaida utambulika kuwa mikondo ya mapato inayofuata ijumuhishwe na:

- Kibali cha uzalishaji cha serikali mwenyeji
- Kibali cha uzalishaji cha kampuni inayomilikiwa na serikali
- Kodi ya faida
- Mlahaba

- Gawio
- Malipo ya ziada (kama sahihi, ugunduzi, uzalishaji)
- Ada ya leseni, kodi ya nyumba, malipo ya kiingilio, na maamuzi mengine kwa leseni na/au makubaliano mengineyo.
- Faida ya mafuta
- Manufaa mengineyo ya muhimu kwa serikali ilivyokubaliwa na kundi la wadau mbalimbali.

Ushahidi: Hili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi ambao kundi la wadau mbalimbali walitoa ushauri katika uendelezaji wa violezo, wajumbe wengi walikuwa na nafasi ya kuchangia, na hivyo kundi la wadau mbalimbali walikubaliana na violezo vya mwisho. Hii ingeweza kujumuhisha ushahidi ufuatao:

- Nakala ya kwanza ya mfumo uliotolewa kwa kundi la wadau mbalimbali
- Muda wa majadiliano wa kiolezo na kundi la wadau mbalimbali
- Mawasiliano kwa wadau mbalimbali (mfano kampuni) kuhusiana na ubunifu wa violezo
- Mipango kuwezesha wadau kufahamu suala lihusikalo
- Makubaliano na kundi la wadau mbalimbali waliokubali violezo, ikijumuhisha mkondo wa mapato kujumuishwa.

Mfumo wa Viashiria 10: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Kundi la Wadau mbalimbali limeridhia na shirika lililoteuliwa kulinganisha mahesabu?

Dhumuni: Shirika litahijika kuteuliwa kupokea mahesabu ya serikali na kampuni zilizofichuliwa, na kutoa taarifa ya mwisho ya EITI. Hili shirika ni maarufu kama Mtawala, Mlinganishaji, au mkaguzi wa hesabu za fedha. Ni muhimu kuwa hii kazi inafanywa na shirika ambalo limeanzishwa na wadau kuwa aminifu na lenye kutegemewa, na lenye uwezo kiufundi.

Ushahidi: Hili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi ambao kundi la wadau mbalimbali limeridhia na shirika lililoteuliwa kulinganisha mahesabu. Hii ingeweza kujumuhisha ushahidi ufuatao:

- Hadidu za rejea zilizokubaliwa na kundi la wadau mbalimbali
- Uwazi ulioshirikisha Sekretarieti ya EITI na Bodi kutambua Wathibiti tegemewa.
- Makubaliano na kundi la wadau mbalimbali kwa chaguo la mwisho la shirika

Mfumo wa Viashiria 11: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Serikali imethibitisha kampuni zote zitatoa taarifa?

Dhumuni: vigezo vya EITI vinahitaji kuwa kampuni zote – Uma (zinazomilikiwa na serikali), binafsi, kigeni na nyumbani- kutaarifu malipo serikalini, kufuatana na mifumo, kwa kampuni lililoteuliwa kulinganisha

mahesabu yaliyofichwa. Serikali itahitaji kuchukua tahadhari zote muhimu kuhakikisha kampuni zote zinataarifu. Haya yaweza kuhusisha utumiaji wa makubaliano ya hiari, utaratibu au sheria. Inatambulika kuwa kunawezeka kukawa na sababu nzuri (japokuwa za kipekee) kwanini baadhi ya kampuni haziwezi kulazimishwa kutoa taarifa katika kipindi kifupi. Katika hali hii, serikali lazima ionyeshe kuwa imechukua hatua madhubuti kuanzisha hizi kampuni kwenye mchakato wa kutaarifu katika kipindi cha kati, na hivyo hizi hatua zitakubalika kwa kampuni nyingine.

Ushahidi: Hili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi ambao serikali imefanya kimoja kati ya vifuatavyo:

- Sheria iliyotangulizwa/rekebishwa inaifanya kuwa na mamlaka kuwa kampuni itataharifu kufuatana na vigezo vya EITI na violezo vilivyokubaliwa.
- Kanuni husika zilizotangulizwa/rekebishwa inaifanya kuwa na mamlaka kuwa kampuni itataharifu kufuatana na vigezo vya EITI na violezo vilivyokubaliwa.
- Makubaliano yaliyofikia muafaka (Kama Tamko la maelewano na hati ya mashtaka ya sharti la siri chini ya makubaliano ya ubia katika uzalishaji) na kampuni zote kuhakikisha zinataarifu kama ilivyoanishwa katika vigezo vya EITI na violezo vya kutoa taarifa.
- Ambapo kampuni hazijashirikishwa, serikali inachukua hatua zilizotambuliwa (na wadau wengine) kiujumla kuhakikisha kampuni hizi zinataarifu tarehe kama ilivyokubaliwa (na wadau).

Mfumo wa Viashiria 12: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Je serikali imehakikisha kuwa msingi wa ripoti za makampuni ni akaunti zilizokaguliwa katika viwango vya kimataifa?

Dhumuni: Vigezo vya EITI vinahitaji kuwa data zote zilizotolewa na kampuni zinahusiana na data zilizochukuliwa kutoka kwenye akaunti ambazo zimekaguliwa kwa kiwango cha kimataifa. Hii ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa EITI.

Ushahidi: Ili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi ambao serikali imechukua hatua kuhakikisha data zilizowasilishwa na kampuni zimekaguliwa kwa viwango vya kimataifa. Hii ingeweza kujumuhisha ushahidi ufuatao:

- Serikali kupitia sheria zinazohitaji mahesabu hili ziwasilishwe kwa viwango vya kimataifa.
- Serikali kurekebisha viwango vya ukaguzi vilivyopo kuhakikisha vipo kwenye viwango vya kimataifa, na vinahitaji kampuni kuvifuata.
- Kampuni kwa hiari kuhaidi kuwasilisha mahesabu yaliyokaguliwa kimataifa.
- Endapo kampuni hazitawasilisha mahesabu yaliyokaguliwa kwa viwango vya kimataifa, serikali imekubaliana mpango na kampuni (unajumuisha SOE) hili kupata viwango vya kimataifa vinavyoharakisha na kuendana na muda/ratiba uliowekwa.

- Endapo mahesabu yaliyotolewa kwa ulinganisho hayapo katika viwango vilivyokaguliwa, kundi la washikadau mbalimbali uridhia njia iliyokubaliwa ya kukabili hili.

Mfumo wa Viashiria 13: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Je serikali imehakikisha kuwa msingi wa ripoti za makampuni ni akaunti zilizokaguliwa katika viwango vya kimataifa?

Dhumuni: Vigezo vya EITI vinahitaji kuwa data zote zilizotolewa na kampuni zimekaguliwa kwa kiwango cha kimataifa.
Ushahidi: Hili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi ambao serikali imechukua hatua kuhakikisha data zilizowasilishwa zimekaguliwa kwa viwango vya kimataifa. Hii ingeweza kujumuhisha ushahidi ufuatao:

- Serikali kupitia sheria zinazohitaji mahesabu hili ziwasilishwe kwa viwango vya kimataifa.
- Serikali kurekebisha viwango vya ukaguzi vilivyopo kuhakikisha vipo kwenye viwango vya kimataifa, na huakikisha vinafuatwa.
- Endapo mahesabu yaliyotolewa kwa ulinganisho hazipo katika viwango vilivyokaguliwa, kundi la wadau mbalimbali uridhia njia iliyokubaliwa ya kuliwasilisha hili.

Mfumo wa Viashiria 14: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Taarifa ya EITI iliwekwa wazi kwa wananchi kwa namna ambavyo ilikuwa?

- Yenye kufikiwa na wananchi,
- Yakinifu, na
- Ya kueleweka?

Dhumuni: Hatimaye taarifa ya EITI itakuwa imetekelezwa kwa ukamilifu itakapokuwa wazi kwa wananchi, na imesambazwa kwa wingi na kujadiliwa wazi na bodi yenye wadau mbalimbali. Vigezo vya EITI kuhitaji kuwa taarifa iko wazi kwa wananchi katika namna ambayo inafikiwa na wananchi, yakinifu na ya kueleweka.

Ushahidi: Hili kukipa kiashirio hiki vema, mthibiti atahitaji kuona ushahidi kuwa serikali imehakikisha taarifa iko wazi kwa wananchi katika namna ambayo inayoendana na vigezo vya EITI, vinajumuhishwa na:

- Kutoa nakala ya karatasi za taarifa, ambazo zimegaiwa kwa wadau mbalimbali, wanaojumuisha vyama vya ushirika, kampuni, vyombo vya habari na wengineo.
- Kuweka taarifa kwenye mtandao, na kuwajulisha anwani ya mtandao wadau muhimu.
- Kuhakikisha kuwa taarifa ni yakinifu, inajumuhisha maelezo yote yaliyokusanywa kama sehemu ya mchakato wa uthibitishaji na mapendekezo yote ya uboreshaji.

- Kuhakikisha kuwa taarifa inaeleweka, inajumuhisha kwa kuhakikisha imeandikwa sawa, kwa staili inyoeleweka na katika lugha inayofaa.
- Kuhakikisha kuwa matukio yanafanikiwa – hata kama yameandaliwa na serikali, vyama vya ushirika au kampuni-vinathibitishwa kutawanya uelewa wa ripoti.

7. Fomu za Kampuni

Mfumo wa Viashiria: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Jinsi gani kampuni za mafuta, gesi na madini zimesaidia utekelezaji wa EITI?

Dhumuni: Kwa kufuatana na kanuni na vigezo vya EITI, kampuni zote zinazofanya kazi katika sekta husika nchini zinazotekeleza EITI zinabidi kufichua malipo ya bidhaa muhimu serikalini kufuatana na violezo vilivyokubaliwa na kusaidia utekelezaji wa EITI. Hii inajumuhisha: kuzihirisha msaada wa uma kwa mkakati; shiriki, au kusaidia, mchakato wa wadau mbalimbali; kufichua data zilizokubaliwa, ambazo zimekaguliwa kwa viwango vya kimataifa; na shirikiana na mthibiti endapo watakuwa na maswali juu ya fomu za kampuni.

Ushahidi: Kiashirio hiki hakitaji Mthibiti kutoa tathmini ya jumla. Mthibiti atatoa tathmini andishi katika taarifa ya uthibitisho ya EITI ihusishayo fomu za kampuni yenyewe zilizotathminiwa (chini) ambayo kila kampuni inahitajiwa kujaza. Endapo kampuni haitajaza fomu, Mthibiti atandika katika taarifa ya mwisho. Pamoja na hayo, Mthibiti itajumuhisha katika taarifa ya mwisho maelezo yoyote yaendanayo juu ya kampuni husika ambayo tayari ipo kwenye himaya ya uma. Kampuni itapewa nafasi ya kucheki haya maelezo. Vilevile kutumia fomu kufupisha utendaji wa kampuni katika taarifa ya EITI, fomu lazima ziwepo kwa uma na

jedwali linalounganisha wito wa kampuni zijumuhishwe katika taarifa ya EITI.

Mthibitishaji atawajulisha kampuni zote zilizohitajika kujaza fomu mwanzoni mwa uthibitishaji, kuwafahamisha vitu vinavyotakiwa kwenye kujaza fomu na kusihi kuwa fomu zitarudishwa kwa Mthibiti. Pamoja na hayo, mthibiti atauliza kampuni kutoa maoni kwa somo lilifunzwa na utendaji bora. Kampuni zitakuwa na namna mbili ya kutoa maoni kama hayo:

- Kampuni zaweza kutumia nafasi iliyopo kwenye fomu za tathmini binafsi, au
- Kampuni yaweza kutoa ushahidi wa maneno kwa Mthibiti anapojadili kampuni atakapofahamu ni yenye asili ya unyeti. Mthibiti atafupisha somo lisilojulikana na kuweka katika taarifa ya uthibitisho.

Fomu ya tathmini binafsi haina budi kujazwa kwa mara ya kwanza na kampuni, kama ifuatavyo:

Ngazi ya Nchi:

- Kila kampuni ya mafuta, gesi au madini inayofanya kazi nchini iliyothibitishwa lazima ijaze fomu ya ngazi ya nchi kama tathmini binafsi na iwasilishwe kwa Mthibiti.
- Mtathmini wa taifa ataunganisha majibu na anaweza kuwasiliana na kampuni kama zina maswali ya ziada au zinahitaji maelezo ya kusaidia zaidi. Kampuni lazima zitikie sawasawa kwa ombi kama hilo.

- Kampuni lazima zitengeneze fomu za utendaji kwa kila nchi ziwepo wazi kwa wananchi kwenye mitandao yao ya nje.

Ngazi ya Kimataifa:

- Kampuni ambazo zimeafiki makubaliano ya kimataifa kusaidia EITI lazima wajaze katika fomu ya tathmini binafsi ya kimataifa.
- Fomu ya kampuni ya kimataifa haina budi kujazwa na kila kampuni na kutumwa kwa sekretarieti ya EITI ambayo wataiweka kwenye mtandao.
- Kampuni zitatoa pia uidhinisho dhahili wa EITI kweye mtandao.

Fomu ya Kampuni ya Uthibitisho wa EITI

Ngazi ya Nchi		
KAMPUNI:	**Nchi:**	
Weka alama ya √ kwenye viashirio chini	Ndiyo	Hapana
1. Kampuni imetengeneza maelezo kwa uma katika usaidizi wa EITI nchini humu? 2. Kampuni imekubali kusaidia na kushiriki katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa EITI wa Nchi (kama ilivyokubaliwa na kundi la wadau mbalimbali), inajumuhisha maagizo yaliyoshikiliwa na selikali yanayohusiana na EITI (kwa mfano:sheria na tamko la maelewano) na, inapobidi, kukutana na wadau? 3. Malipo yote ya bidhaa yamefichuliwa katika shirika lilokubaliwa kulinganisha mahesabu na kutoa taarifa ya EITI kama ilivyokulibaliwa katika violezo vya EITI na kufuatilia kwenye muda uliokubaliwa? 4. Data zilizowasilishwa kwenye shirika lilokubaliwa kulinganisha mahesabu na kutoa taarifa ya EIT iliyochukuliwa kwenye akaunti ambayo imekaguliwa kwa kutotegemeana na viwango vya kimataifa? 5. Kampuni imekubali maswali kutoka katika shirika lilokubaliwa kulinganisha mahesabu na kutoa taarifa ya EITI kusaidia katika ulinganishaji wa malipo ya nchi na risiti za serikali kwa kufuatana na violezo vya kutaarifu vya EITI?		
	Ndiyo	Hapana
Tathmini ya Jumla (ya hayo juu)		

Maoni Simulizi.	
Kama kiashirio chochote juu vimewekewa ‘hapana’ tafadhali toa maelezo.	
Maoni mengineyo.	

Ngazi ya Kimataifa		
KAMPUNI:		
Weka alama ya √ kwenye viashirio chini	Ndiyo	Hapana
1. Kampuni imechapisha maelezo ya wazi yanayoidhinisha kanuni na vigezo vya EITI, na kuakikisha inapatikana kwenye mtandao wa nje? 2. Iwapo itatumika (kama vile kwa utendaji katika nchi zinazotekeleza EITI ambazo angalau zimemaliza uthibitishaji mmoja), kampuni imetoa anwani katika mtandao wake wa nje kwa fomu za kampuni zilizojazwa? 3. Kampuni imepewa majukumu ya mikakati? Ya EITI kwa wahusika wa juu wa utawala na kuteua kiongozi inayehusika na mawasiliano ya sera za EITI ya kampuni, kufuatilia usaidizi wa EITI, na kukubali maswali kutoka kwa wadau wa EITI? 4. Iwapo Mkutano wa kimataifa umefanyika katika kipindi cha uthibitishaji, je wahusika wa uongozi wa juu waliudhuria au walituma maelezo saidizi? 5. Endapo Kampuni ina taarifa ya uendelevu ya Dunia au taarifa ya majukumu shirikishi, kampuni imejumuhisha muhtasari wa mchango wake kwa EITI katika hili na kwenye mtandao wake wa nje?		
	Ndiyo	Hapana
Tathmini ya Jumla (vya juu)		

Maoni Simulizi.	
Kama kiashirio chochote juu vimewekewa 'hapana' tafadhali toa maelezo.	
Maoni mengineyo.	

8. Kiashirio cha Mapitio

Mfumo wa Viashiria: Chombo cha Kiashirio cha Tathmini

Kiashirio: Hatua gani zimechukuliwa kufuatilia somo lililofunzwa, kukabili itilafu na kuhakikisha utekelezaji wa EITI ni endelevu?

Dhumuni: Uzalishaji na usambazaji wa taarifa ya EITI sio mwisho wa utekelezaji wa EITI. Thamani inatoka kwenye mchakato zaidi ya zao, na ni muhimu kuwa mafundisho yaliyofunzwa katika utekelezaji wa EITI yanafuatiliwa, itilafu zilizotambuliwa katika Taarifa ya EITI zimekabiliwa na hivyo utekelezaji wa EITI upo juu ya msingi imara na endelevu.

Ushahidi: Mthibiti ataona ushahidi kuwa njia za mapitio zimeundwa endapo madhumuni yaliyotolewa juu yamezingatiwa.